## Wasaiedie Watoto Wako Wakae Salama...

- Ongea.
- Uliza Maswali.
- Sikiliza.
- Jihusishe katika maisha yao ya Shule.
- Jua marafiki wake.
- Kua mwangalifu kwa mabadiliko ya dharura ya tabia, matokeo ya shule, au manufaa ya.
- Ukihitaji usaidizi, wasiliana na utekelezaji wa sheria au wasimamizi wa shule kwa usaidizi. Wahimize watoto wako wafanye hivyo.





**Idara ya Polisi ya Bowling Green**

Mtaa wa Kentucky 911
Bowling Green, KY 42101
Nambari ya simu: 270-393-4244
www.bgky.org/police

Shule za Jiji la Bowling Green
Nambari ya simu: 270-746-2200
www.b-g.kyschools.us
Shule za Mkoa wa Warren
Nambari ya simu: 270-781-5150
www.warren.kyschools.us
Afisi ya Mkoa ya Sheria ya Warren
Nambari ya simu: 270-782-2760
Afisi ya Jumuiya ya madola ya Sheria
Nambari ya simu: 270-746-7485
Idara ya Mkoa ya Afya ya Barren River
Nambari ya simu: 270-781-2490 Uenezi. 214

Kwa dharura: Piga 911

©1998-2009 Jiji la Bowling Green haki zote zimehifadhiwa.

# *Kuwaweke Watoto wako Salama*

## Mwongozo wa Sheria za Kentucky za Wakimbizi na Wazazi wa Wahamiaji

Chapisho Limetolewa na Idara ya Polisi ya Bowling Green ikishirikiana na Jiji la Bowling Green na Mifumo ya Shule za Mkoa za Warren; Mkoa wa Warren na Afisi ya Sheria ya Jumuiya ya madola; na Idara ya Afya ya Wilaya ya Barren River.

*Sehemu imedhaminiwa na Afisi ya KY ya Wakimbizi, Shule ya Wakimbizi ya Usaidizi ya Mawasiliano, Afisi ya kuwapa wakimbizi makaazi,HHS*

(Swahili)

# Barua kwa wazazi wahamiaji...

Vijana Wakimbizi na Wahamiaji wanakabiliwa na hatari nyingi wakati hao ni wageni katika nchi na jumuia. Baadhi ya hatari hizo ni sawa na zile mtoto yoyote anakabiliwa nazo wakati anapohamia mahali pageni, kuwa na marafiki wapya, na kwenda katika shule mpya. Lakini kwa mkimbizi na watoto wahamiaji, changamoto maalum na shida zipo. Utamaduni na shida za lugha zaweza kusababisha mtoto ajihisi mpweke, kutamani nyumbani, kutengwa, na peke yake. Hisia hizo zaweza kusababisha watoto kutafuta urafiki mahali pasipo faa na kwa watu wasiofaa. Na matokeo kuwa, wanakuwa katika hatari ya kujiunga na makundi ya wahuni, mlevi wa madawa na taathira ya ulevi, na ngono, na hatari zingine. Kama mzazi, ni muhimu kwako kujua majukumu yako na sheria zilizoundwa kuwalinda watoto wako katika jimbo la Kentucky.



## Baadhi ya Sheria za Kentucky ambazo zinawalinda watoto wako...

*"Kuhatarisha Ustawi wa mtoto mdogo," Sheria ya Kentucky (KRS 530,060)* inasema kuwa mzazi au mlezi lazima amchunge mvulana au msichana wake kutokana na kutotunza, kuepika kutelekeza, au mtoto mhalifu.

*"Ni kinyume cha sheria kuendesha Biashara na Mtoto mdogo." Sheria ya Kentucky (KRS 530.064; 530.065; 530.070)* inasema ya kwamba ni kinyume cha sheria kumpembeja, kusaidia, au kumfanya mtoto mdogo kujihusisha na kitendo cha ngono kisicho halali , utumizi mbaya wa dutu ikijumuisha bangi, kumpa mtoto mdogo pombe; kumpa mtoto mdogo motisha ya kujihusisha na kitendo cha jinai, mtoro kutoka shule, au kutomheshimu mzazi wake au mlezi.

*"Kusajiwa kwa Kundi la Jinai;" Sheria ya Kentucky ( KRS 506,140)* inasema ya_ kwamba ni kinyume cha sheria kwa mtu yeyote kuomba au kulaghai mtu kujiunga na kundi au kuogofya au kutisha mtu yeyote kwa kukataa kujiunga, kwa kujitoa, au kwa kukataa kuafikiana na mahitaji yalio wekwa na kundi.

*Sheria 91 ya Bunge: Kanuni Muhimu* sheria ya Kentucky ya 2008 ilio rejelewa mara kadhas ya kuimarisha hatua zitakazo chukuliwa na wasimazi wa shule na utekelezaji wa sheria dhidi ya wanafunzi wanao dhulumu au kusumbua wanafunzi wengine.



## Sheria za Kentucky Dhidi ya Makosa ya Ngono Yanayo Jumuisha Watoto...

Sheria nyingi za Kentucky zinakabiliana na makosa ya ngono, ikijumuisha na isiyokua na kikomo kwa Sheria zilizo rejelewa za Kentucky 510.040, 510.050, na 510.060. Sheria hizi ziko tofauti kutoka na pia haziko katika nchi nyingi duniani. Ni muhimu kabisa kujua hivyo kulingana na Sheria ya Kentucky ya kuwa, mtoto chini ya miaka 16 haruhusiwi kukubali tukio lolote la ngono.

Kwa hivyo, ni haramu kwa mtu yeyote kufanya mapenzi na mtu yeyote wa chini ya miaka 16.

*Kwa habari zaidi kuhusu haya na sheria zingine za Kentucky, tembelea mtandao ufuatao:*

*www.lrc.ky.gov*

*au wasiliana na ajenti yoyote aliye orodheshwa katika kijitabu hiki.*

